Mganga Mkuu

na

Ellis P. Forsman

Mganga Mkuu

na

Ellis P. Forsman

Oktoba 7, 2011

Mganga Mkuu

Marko 2:1-17

Marko 2:1-17, *"Akaingia kapernaumu tena baada ya siku kadha wa kadha ikasikiwa ya kwamba yumo nyumbani. Wakakusanyika watu wengi isibaki nafasi hata mlangoni akawa akisema nao neno lake. Wakaja watu wakimletea mtu mwenye kupooza ana chukuliwa na watu wane. Na walipokuwa hawawezi kumkaribia kwa sababu ya makutano, walitoboa dari pale alipokuwapo na wakiisha kulivunja wakalitelemsha godoro alilolilalia yule mwenye kupooza. Naye Yesu, alipoiona imani yao akamwambia Yule mwenye kupooza, Mwanangu umesamehewa dhambi zako. Na baadhi ya waandishi walikuwamo huko, wameketi wakifikiri mioyoni mwao. Mbona huyu anasema hivi? Anakufuru. Ni nani awezaye kusamehe dhambi isipokuwa mmoja, ndiye Mungu? Mara Yesu akafahamu rohoni mwake kwamba wanafikiri hivyo nafsini mwao, akawambia mbona mnafikiri hivi mioyoni mwenu? Vyepesi ni vipi, kumwambia mwenye kupooza, Umesamehewa dhambi zako au kusema, ondoka ujitwike godoro lako uende? Lakini mpate kujua ya kwamba Mwana wa Adamu anayo amri duniani ya kusamehe dhambi, (hapo amwambia Yule mwenye kupooza), nakuambia ondoka ujitwike goro lako uende nyumbani kwako. Mara akaondoka akajitwika godoro lake, akatoka mbele yao wote; hata wakastaajabu wote, wakamtukuza Mungu, wakisema, namna hii hatujapata kuiona kamwe. Akatoka tena akaenda kando ya bahari, mkutano wote ukamwendea akawafundisha. Hata alipokuwa akipita akamwona Lawi wa Alfayo, ameketi forodhani, akamwambia nifuate. Akaondoka akamfuata. Hataalipokuwa ameketi chakulani nyumbani mwake watoza ushuru wengi na wenye dhambi waliketi pamoja na Yesu na wanafunzi wake; kwa maana walikuwa wengi wakimfuata. Na Wandishi na Mafarisayo walipomwona anakula pamoja na watoza ushuru na wenye dhambi, waliwambia wanafunzi wake mbona anakula pamoja na watoza ushuru na wenye dhambi? Yesu aliposikia aliwambia, wenye afya hawaitaji tabibu, bali walio hawawezi; sikuja kuwaita wenye haki, bali wenye dhambi."*

Mtu anapokuwa mgonjwa mara nyingi anamtafuta daktari amchunguze kuhusiana na ugonjwa wake. Alafu daktari anatoa matibabu halisi na namna ya kutumia dawa, au kutoa maelekezo ya kumhudumia mgonjwa huyo.

Daktari lazima awe na upeo mkubwa wa uelewa wa magonjwa tofauti na matibabu ili kuifanya kazi yake vyema. Kama daktari akitoa maelezo ya dawa zisizo ponya kwa ajilia ya ugonjwa ambao haupo, matokeo yatakuwa ni hatari.

Wakati mwingine kwa sababu ya kazi alizonazo nyingi, anatoa maelekezo kwa wengine ili kutekeleza: manesi, wanaotoa mwongozo, wagawa madawa, nk. Hawa hawawezi kufahamu mengi kama daktari anavyojua, lakini wanapaswa kujua mengi kama wakifuata maelekezo yake.

Miaka kadhaa nililazwa hospitalini kwa ajili ya tatizo la moyo. Wafanya kazi wa hospitali hiyo na wanaohusika katika magari ya kubebea wagonjwa walifikiri nina ugonjwa wa moyo. Daktari wa moyo akasema nilikuwa ninajaribu kuwa na mshituko wa moyo, na si ugonjwa wa moyo. Alitaka niendelee kukaa hospitalini kwa majaribio zaidi na akataka nimeze madawa ili inisaidie katika kiwango cha moyo. Usiku nilipokuwa nina lala, nesi alikuwa ana angalia kifaa kilicho shikishwa kwangu aliniamsha na kuniuliza, “Bwana. Forsman, unajisikiaje?” Nikasema kulikuwa na mshituko mdogo katika kifua, lakini si kama ilivyokuwa nilipokuwa nime lazwa. Akanipa kitu Fulani kwenye mkono, ghafla masikio yangu yalikuwa yanaunguruma, kichwa kilikuwa kinazunguka, na nilijisikia vibaya katika mwili wangu wote. Nikasema, “Nini kinachoendelea?” nilipokuwa nikitafakari hisia zangu. Akasema. “Usijali kuhusu hilo; hiyo inasababishwa na madawa niliyokupa. Dakika wa tano baadaye, manesi wane zaidi wakafika chumbani, nikapata tena sindano nyingine katika mkono ule ule ambayo walichoma sindano ya kwanza na adhari kama za awali. Kitu kilichofuata nilichokijua, walikuwa wananisukuma katika vitanda vya wagonjwa mahututi kwenye korido wakinipeleka kwenye chumba cha tahadhari ambapo uangalizi mwingi uliwekwa kwangu. Siku iliyofuata daktari wangu akaja chumbani kwangu na kuniuliza, “Unafanya nini katika chumba hiki?” Nikasema, “Sijui; waulize manesi.” Akaangalia karatasi la maelezo ya wagonjwa lililotundikwa pembezoni mwa kitanda, akaitoa na kukimbia kwenda katika ofisi ya manesi. Nikamsikia anapiga kelele, “Kama hamkujua mlichokuwa mnakifanya kwa nini hamkunipigia simu? Mmempa matibabu ya ugonjwa wa moyo; yeye si mgonjwa wa moyo; alikuwa tu na jaribio dogo!” Uwazi, hawakujua mengi kama daktari alivyojua.

Tuna daktari mkuu ni Yesu Kristo anayejua matatizo yote ya ulimwengu na matibabu yake.

- Yoh. 2:24-25, *“Lakini Yesu hakujiaminisha kwao kwa kuwa yeye aliwajua wote; na kwa sababu hakuwa na haja ya mtu kushuhudia habari za mwanadamu; kwa maana yeye mwenyewe alijua yaliyomo ndani ya mwanadamu.”*
- Yoh. 1:3, *“Vyote vilifanyika kwa huyo wala pasipo yeye hakikufanyika chochote kilichofanyika.”*

- Marko 2:13-17, *"Akatoka tena akaenda kando ya bahari mkutano wote ukamwendea akawafundisha. Hata alipokuwa akipita alimwona Lawi wa Alfayo ameketi forodhani akamwambia, nifuate. Akaondoka akamfuata. Hata alipokuwa ameketi chakulani nyumbani mwake watoza ushuru wengi na wenye dhambi waliketi pamoja na Yesu na wanafunzi wake; kwa maana walikuwa wengi wakimfuata. Na waandishi na Mafarisayo walipomwona anakula pamoja na watoza ushuru na wenye dhambi, waliwaambia wanafunzi wake, mbona anakula pamoja na watoza ushuru na wenye dhambi? Yesu aliposikia aliwambia, Wenye afya hawaitaji tabibu, bali walio hawawezi, sikuja kuwaita wenye haki, bali wenye dhambi."*

Yesu amewaagiza wengine kuendeleza kazi yake, kama jinsi daktari anavyotoa maelekezo kwa manesi.

Mitume.

Math. 28:16-20, *"Na wale wanafunzi kumi na mmoja wakaenda Galilaya mpaka mlima ule aliowaagiza Yesu. Nao walipomwona, walimsujudia; lakini baadhi yao waliona shaka. Yesu akaja kwao akasema nao akawaambia nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Basi enendeni mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi mkiwabatiza kwa jina la Baba na la mwana na la Roho Mtakatifu, na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari."*

Wengine.

2 Tim. 2:2, *"Na mambo yale uliyoyasikia kwangu mbele ya mashahidi wengi hayo uwakabidhi watu waaminifu watakaofaa kuwafundisha na wengine."*

Ugonjwa ni nini? Dhambi.

Isa. 1:2-6, *"Sikieni enyi mbingu, tega sikio Ee nchi kwa maana BWANA amenena, nimewalisha watoto na kuwalea, nao wameniasi. Ng'ombe amjua bwana wake na punda ajua kibanda cha bwana wake; Bali Israeli hajui, watu wangu hawafikiri. Ole wake taifa lenye dhambi, watu wanaochukua mzigo wa uovu wazao wa watenda mabaya watoto wanaharibu wamemwacha BWANA, wamemdharau yeye aliye mtakatifu wa Israeli, wamefarakana naye na kurudi nyuma. Mbona mnataka kupigwa hata sasa, hatamkazidi kuasi? Kichwa chote ni kigonjwa, moyo wote umezimia. Tangu wayo wa mguu hata kichwani hamna uzima ndani yake; balijeraha na machubuko na vidonda vitokavyo usaha,*

havikufungwa havikuzongwa- zongwa wala havikulainishwa kwa mafuta."

Ni Ugonjwa unaouwa.

- Waru. 8:13, *"Kwa maana kama tukiishi kwa kufuata mambo ya mwili, mwataka kufa, bali kama mkiyafisha matendo ya mwili kwa Roho, mtaishi."*
- Yako. 1:14-15, *"Lakini kila mmoja hujaribiwa na tama yake mwenyewe huku akivutwa na kudanganywa. Halafu ile tamaa ikiisha kuchukua mimba huzaa dhambi, na ile dhambi ikiisha kukomaa huzaa mauti."*
- Yako. 5:19-20, *"Ndugu zangu ikiwa mtu wa kwenu amepotelea mbali na kweli na mtu mwingine akamrejeza; jueni ya kuwa yeye amrejezaye mwenye dhambi hata atoke katika njia ya upotevu, ataokoa roho na mauti, na kufunika wingi wa dhambi."*

Dunia nzima inaumwa

- Mhubiri 7: 20, *"Bila shaka hakuna mwanadamu mwenye haki hapa duniani; ambaye afanya mema asifanye dhambi."*
- Waru. 3: 9-10, *"Ni nini basi? Tu bora kuliko wengine? La! Hata kidogo. Kwa maana tumekwisha kuwashitaki Wayahudi na Wayunani ya kwamba pia wamekuwa chini ya dhambi. Kama ilivyoandikwa ya kwamba, hakuna mwenye haki hata mmoja. "*

Dawa lazima imezwe ili itibu

- Waru. 6:16-17, *"Hamjui ya kwamba kwake yeye ambaye mnajitoa nafsi zenu kuwa watumwa wake katika kumtii, mmekuwa watumwa wake Yule mnayemtii, kwamba ni utumishi wa dhambi uletao mauti, au kwamba ni utumishi wa utii uletao haki. Lakini Mungu na ashukuriwe, kwa maana mlikuwa watumwa wa dhambi, lakini mliitii kwa mioyo yenu ile namna ya elimu ambayo mliwekwa chini yake."*
- 1 Petr. 1:22-25, *"Mkiisha kujitakasa roho zenu kwa kuitii kweli, hata kuufikilia upendano wa ndugu usio na unafiki, basi jitahidini kupendana kwa moyo. Kwa kuwa mmezaliwa mara ya pili; si kwa mbegu iharibikayo; kwa neno la Mungu lenye uzima, lidumulo hata milele. Maana mwili wote ni kama majani, na fahari yake yote ni kama ua la majani. Majani hukauka na ua lake hukauka; Bali neno*

la Bwana hudumu hata milele. Na neno hilo ni neno lile jema lililohubiriwa kwetu."

Kunywa kama ilivyoagizwa.

Ni hatari kunywa dawa wakati alama au maelezo ya kwenye chupa hayapo.

- Je unahakika ni matibabu sahihi?
- Je unahakika ni dawa nzuri.

Usimruhusu meingine abadilishe matibabu yaliyotolewa na daktari.

- Wagal. 1:6-9, *"Nastaajabu kwa kuwa mnamwach upesi hivi yeye aliyewaita katika neema ya Kristo, na kugeukia injili ya namna nyingine. Wala si nyingine, lakini wapo watu wawataabishao na kutaka kuigeuza injili ya Kristo. Lakini ijapokuwa sisi au malaika wa mbinguni atawahubiri ninyi injili yoyote isipokuwa hiyo tuliyo wahubiri, na alaaniwe. Kama nilivyotangulia kusema, na sasa nasema tena, mtu awaye yote akiwahubiri ninyi injili yoyote isipokuwa hiyo mliyoipokea na alaaniwe."*
- 2 Yoh. 1:9-10, *"Kila apitaye cheo wala asidumu katika mafundisho ya Kristo, yeye hana Mungu. Yeye adumuye katika mafundisho hayo, huyo ana Baba na Mwana pia. Mtu akija kwenu, naye haleti mafundisho hayo, msimkaribishe nyumbani mwenu, wala msimpe salamu."*

Wakati mwingine daktari anaweza kupendekeza chakula kamili, mazoezi, au mazingira tofauti

- 1 Petr. 2:2, *"Kama watoto wachanga walio zaliwa sasa, yatamanini maziwa ya akili yasioghoshiwa ili kwa hayo mpate kuukulia wokovu."*
- Matend. 20:32, *"Basi sasa nawaweka katika mikono ya Mungu na kwa neno la neema yake, ambalo laweza kuwajenga na kuwapa urithi pamoja nao wote waliotakaswa."*
- 1 Tim. 4:7-8, *"Bali hadithi za kizee zisizokuwa za dini, uzikatae; nawe ujizoeze kupata utaua. Kwa maana kujizoeza kupata nguvu za mwili kwafaa kidogo lakini utaua hufaa kwa mambo yote; yaani unayo ahadi ya uzima wa sasa, na ule utakaouwapo baadaye."*
- 1 Wakor.15:33, *"Msidanganyike mazungumzo mabaya huaribu tabia njema."*

- 1 Wakor. 4:6-7, *"Basi ndugu zangu mambo hayo nimeyafanya kuwa mfano wa mimi na Apolo kwa ajili yenu, ili kwamba kwa mfano wetu mpate kujifunza kutokupita yale yalioandikwa ili mmoja wenu asijivune kwa ajili ya huyu, kinyume cha mwenziwe. Maana ni nani anayekupambanua na mwingine? Nawe una nini usichokipokea? Lakini iwapo ulipokea wajisifia nini kama kwamba hukupokea."*

Watu wengi ni wagonjwa kwa ugonjwa wa kufikiria

Madaktari maofisa watu wanajaa kwao kwa sababu wanafikiria ni wagonjwa.

Katika Agano la Kale, Eliya alikuwa kinara mwenye nguvu mpaka akaanza kufikiria kwamba alikuwa ni yeye mwenyewe aliyekuwa akipigana vita. Alafu akakaa chini ili afe.

- 1 Wafalme 19:4, *"Lakini yeye mwenyewe akaendelea katika jangwa mwendo wa siku moja, akaenda akaketi chini ya mretemu. Akajiombea roho yake afe, akasema, yatosha; sasa Ee BWANA, uiondoe roho yangu, kwa kuwa mimi si mwema kuliko baba zangu."*
- 1 Wafalme 19:14, *"Akasema nimeona wivu mwingi kwa ajili ya BWANA, Mungu wa majeshi kwa kuwa wana wa Israeli wameyaacha maagano yako na kuzivunja madhabahu zako na kuwaua manabii wako kwa upanga; name nimesalia, mimi peke yangu; nao waitafuta roho yangu waiondoe."*
- 1 Wafalme 19:18, *"Pamoja na hayo nitajisazia katika Israeli watu elfu saba kila goti lisilomwinamia Baali na kila kinywa kisichombusu."*

Kufikiria ilikuwa ni sehemu ya kuanguka kwa mwanadamu kama jinsi inavyo ongelewa na Paulo. Waru. 1:21, *"Kwa sababu walipo mjua Mungu hawakumtukuza kama ndiye Mungu wala kumshukuru; bali walipotea katika uzushi wao, na mioyo yao yenye ujinga ikatiwa giza."*

Watu wengi wanateseka na magonjwa mbalimbali ambayo huenyesha dalili ya kutetemeka, watu wanapokwa wadhaifu na kushindwa kutimiza mengi

Hii ni kweli kiroho pia. Baadhi wanashindwa kuinua hata mikono yao na magoti yaliyopooza. Waeb. 12:12-13, *"Kwa hiyo inyosheni mikono ililiyolegea na magoti na magoti yaliyopooza, mkaifanyie miguu yenu njia za kunyoka ili kitu kilichokiwete kisipotoshwe, bali afadhali kiponywe."*

Hii husababishwa na ukosefu wa chakula cha kiroho. Waeb. 5:12, *"Kwa maana iwapasavyo kuwa waalimu, (maana wakati mwingi umepita, mnahitaji kufundishwa na watu mafundisho ya kwanza ya maneno ya Mungu, nanyi mmekuwa mnahitaji maziwa wala si chakula kigumu."*

Dawa ya hii ni kurudi katika neno la Mungu na uwe makini na yafuatayo.

- Waeb. 2:1-2, *"Kwa hiyo imetupasa kuyaangalia zaidi hayo yaliyosikiwa tusije tukayakosa. Kwa maana ikiwa lile neno lililonenwa na malaika ilikuwa imarara, na kila kosa na uasi ulipata ujira wa haki."*
- Waeb. 12:1-2, *"Basi na sisi pia kwa kuwa tunazungukwa na wingu kubwa la mashahidi namna hii na tuweke kando kila mzigo mzito na dhambi ile ituzingayo kwa upesi na tupige mbio kwa saburi katika yale mashindano yaliyowekwa mbele yetu, tukimtazama Yesu, mwenye kuanzisha na mwenye kutimiza imani yetu, ambaye kwa ajili ya furaha iliyowekwa mbele yake aliustahimili msalaba na kuidharau aibu, naye ameketi mkono wa kuume wa kiti cha enzi cha Mungu."*

Watu wengi leo wana ugonjwa wa moyo

Moyo unaweza kuwa mzigo.

Math. 13:15, *"Maana mioyo ya watu hawa imekuwa mizito, na kwa masikio yao hawasikii vema, na macho yao wameyafumba; wasije wakaona kwa macho yao, wakasikia kwa masikio yao, wakaelewa kwa miyo yao, wakaongoka nikawaponya."*

Moyo unaweza ukawa mgumu.

Marko. 10:5, *"Yesu akawambia, kwa sababu ya ugumu wa mioyo yenu aliwaandikia amri hii."*

Moyo unaweza kuanza kufikiria visivyo.

Matendo 8:21-22, *"Huna fungu wala huna sehemu katika jambo hili, kwa kuwa moyo wako si mnyofu mbele za Mungu. Basi tubia uovu wako huu, ukamwombe Bwana ili kama yamkini usamehewe fikira hii ya moyo wako."*

Moyo unaweza kuwa kipofu.

Waef. 4:18, *"Ambao akili zao aimetiwa giza nao wamefarikishwa na uzima wa Mungu, kwa sababu ya ujinga uliomo ndani yao, kwa sababu ya ugumu wa mioyo yao."*

Moyo unaweza kudanganyika.

Yak.1:26, *"Mtu akidhani ya kuwa anayo dini, wala hauzuii ulimi wake kwa hatamu hali akijidanganya moyo wake, dini yake mtu huyo haifai."*

Moyo unaweza kuhusika katika mambo yasiyofa.

2 Petr. 2:14, *"Wenye macho yajaayo uzinzi watu wasiokoma kutenda dhambi wenye kuhadaa roho zisizo imara, wenye mioyo iliyozoezwa kutamani, wana wa laana."*

Kuna njia nyingi ambazo mtu anaweza akawa na tatizo la moyo kiroho.

Dawa ni kuutakasa moyo.

- Matendo 15:9, *"Na usiweke tofauti kati yetu na wao, bali utakase mioyo yao kwa imani."*
- Waeb. 10:22, *"Na tukaribie wenye moyo wa kweli, kwa utimilifu wa imani, hali tumenyunyiziwa mioyo tuache dhamiri mbaya, tumeoshwa miili kwa maji safi."*
- Yakobo 4:8, *"Mkaribieni Mungu naye atawakaribia ninyi. Itakaseni mikono yenu enyi wenye dhambi, na kuisafisha mioyo yenu enyi wenye nia mbili."*

Hii inaweza kufanyika kwa kutii injili au kuweka mambo sawa kama mkristo anayepotea

Waru. 6:1-4, *"Tuseme nini basi? Tudumu katika dhambi ili neema izidi kuwa nyingi? Hasha! Sisi tulioifia dhambi tutaishije tena katika dhambi? Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika*

mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima."

Ugonjwa wa kawaida ni wa matatizo ya macho.

Watu wengi wanamatatizo ya macho kiroho.

Baadhi wanafumba macho yao.

Math. 13:15, *"Maana nioyo ya watu hawa imekuwa mizito, na kwa masikio yao hawasikii vema, na macho yao wameyafumba; wasije wakaona kwa macho yao, wakasikia kwa masikio yao, wakaelewa kwa miyo yao,wakaongoka nikawaponya."*

Wengine wanaupofu.

2 Wakor. 4:4, *"Ambao ndani yao mungu wa dunia hii amepofusha fikira zao wasioamini isiwazukie nuru ya injili wa utukufu wake Kristo aliye sura yake Mungu."*

Wengine wana macho maovu.

Math. 6:23, *"Lakini jicho lako likiwa bovu mwili wako wote utakuwa na giza. Basi ile nuru iliyomo ndani yako ikiwa giza; si giza hilo."*

Wengine wanapata ugonjwa wa macho kupitia ukaidi.

Waef. 4:18, *"Macho ya mioyo yenu yatiwe nuru, mjue tumaini la mwito wake jinsi lilivyo, na utajiri wa utukufu wa urithi katika watakatifu jinsi ulivyo."*

Dawa kwa ajili ya tatizo la macho ni kumrudia Kristo

2 Wakor. 3:14-16, *"Ila fikira zao zilitiwa uzito. Kwa maana hata leo hivi wakati lisomwapo Agano la kale, utaji uo huo wakaa yaani haikufunuliwa kwamba huondolewa katika Kristo; ila hata leo torati ya Musa isomwapo utaji huikalia mioyo yao. Lakini wakati wowote watakapomgeukia Bwana, ule utaji huondolewa."*

Alafu utumie dawa yake ya macho.

Ufu. 3:18, *"Nakupa shauri ununue kwangu dhahabu iliyosafishwa kwa moto upate kuwa tajiri na mavazi meupe upate kuvaa, aibu ya uchi wako usionekane, na dawa ya macho ya kujipaka macho yako, upate kuona."*

Mwisho

Yesu Kristo ndiye daktari mkuu. Alikuja kutafuta na kuwaokoa waliopotea.

Luka. 19:10, *"Kwa maana mwana wa Adamu alikuja kutafuta na kuokoa kile kilicho potea."*

Kristo pekee ndiye anayeweza kutoa pumziko la kweli.

Math. 11:28-30, *"Njooni kwangu ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha. Jitieni nira yangu mjifunze kwangu; kwa maana mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo nanyi mtapata raha nafsini mwenu; kwa maana nira yangu ni laini na mzigo wangu ni mwepesi."*

Ni nini ambacho daktari mkuu anatoa kama dawa ya dhambi? Yafuatayo ndio maelekezo aliyotoa:

- **Imani.** Waeb. 11:6, *"Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza; kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko, na kwamba huwapa dhawabu wale wamtafutao."* Nilipokuwa shuleni (nikiwa na miaka 17), kijana mmoja jirani yangu mwaka sawa na mimi akniambia kwamba haamini kwamba Mungu yuko. Kwa vile nilisha batizwa, nilichukua nafasi ya kuongea naye kuhusu mandiko. Akaniambia kwamba anaweza kuona kwamba kuishi maisha ya ukristo ni nzuri, lakini hakuwa na uhakika kwamba Mungu yuko. Lakini ili kuwa upande salama, labda anapaswa kwenda kanisani, na akifa na kusimama mbele za Mungu (kama kuna Mungu) siku ya hukumu (kama kuna hukumu), labda kama Mungu akiona kuwa amekwenda kanisani atampeleka mbinguni (kama kuna mbingu), na si motoni (kama kuna moto). Nikamwambia, "haifanyi kazi kwa njia hiyo. Lazima uamini katika yeye kwa moyo wako wote la sivyo huwezi kumpendeza.

- **Toba.** Matend. 2:38, *"Petro akawambia, tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu kwa jina lake Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi zenu nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu."* Matend 11:18, *".....Basi Mungu amewajalia hata mataifa nao toba liletalo uzima."* Kama ulikuwa unalala, ukasikia kelele kwenye chumba kingine, na unafikiria mwenyewe, "Kwamba kuna mwizi!" taratibu unachukua simu ya mkononi, unawapigia polisi. Kidogo polisi wanafika na kumshika mwizi. Alafu anapiga kelele, "samahani; samahani!" Anaomba msamaha wa nini? Kwa sababu amekamatwa; si kwamba ameiba. Toba iliyokweli ni kwamba mwizi angeomba msamaha kwamba hataiba tena. Hiyo ndio toba ya kweli. Ni badiliko la nia linaloleta badiliko la matendo. Tunatakiwa kufanya hivyo kabla hatujawa wakristo.

- **Kukiri.** Waru. 10:9-10, *"Kwa sababu ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana na kuamini moyoni mwako ya kuwa*

Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu."

Tuna kiri nini? Kwamba tuna amini kwamba Yesu Kristo ni mwana wa Mungu.

Kumbuka kwamba katika andiko hilo hapo juu kwamba imani (kuamini), toba, na kukiri ni "**KATIKA**" haki, uzima, au wokovu. "Katika" inamanisha kuelekeza kwenye kitu Fulani; si kwamba mtu ameshapata.

- **Ubatizo.** Ni katika ubatizo ndipo haki, uzima, na wokovu vinapatikana. Yesu mwenyewe alibatizwa kuitimiza haki yote, *"Lakini Yohana alitaka kumzuia akisema, mimi nahitaji kubatizwa na wewe, nawe waja kwangu? Yesu akajibu akamwambia kubali hivi sasa, kwa kuwa ndivyo itupasavyo kuitimiza haki yote. Basi akamkubali. Naye Yesu alipokwisha kubatizwa mara akapanda kutoka majini, na tazama mbingu zikamfunukia akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua, akija juu yake; na tazama sauti kutoka mbinguni ikisema, huyu ni mwanangu mpendwa, ninaye pendezwa naye."* (Math. 3:14-17). Yesu alibatizwa kwa sababu Mungu alisema ni jambo sahihi la kufanya. Unaona ni jinsi gani ilivyompendeza Mungu Yesu alipobatizwa? Yesu pia akasema, "*Imekuwa kwetu **sisi** kuitimiza haki yote."* Tuna batizwa kwa sababu inatimiza haki yake yote, si kwa sababu ni haki yetu.

  Kwa kweli, tusipo batizwa, tungali katika dhambi zetu. *"Petro akawambia, tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu kwa jina lake Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi, na mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu."* (Matend. 2:38). Petro, umesema kusudi la ubatizo ni nini? "*Kwa ajili ya ondoleo la dhambi*". Kwa nini watu wanapenda kuach hatua inayotuondoa dhambi zetu?

  Yesu aliamuru kwamba ili kuufikia wokovu lazima tubatizwe. *"Na akawambia enendeni ulimwenguni kote mkahubiri injili kwa kila kiumbe. Aaminiye **na** kubatizwa ataokoka; asiyeamini atahukumiwa."* (Marko 16:15-16).

  Anania alimwambia Sauli (kabla hajaitwa Paulo) kitu iki hiki, "*Unakawilia nini? Simama, na ubatizwe, na uoshwe dhambi zako, ukiliitia jina la Bwana."* (Matend. 22:16). Ubatizo ni hitaji lililotolewa na Mungu.

  Ubatizo unaitwa maziko, *"Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima."* (Waru. 6:4). Utu wetu wa kale

umekufa. *"Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake. Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima. Kwa maana kama mlvyounganika naye katika mfano wa mauti yake, kadhalika mtaunganika katika mfano wa kufufuka kwake; mkijua neno hili ya kuwa utuwetu wa kale ulisulubishwa pamoja naye, ili mwili wa dhambi ubatilike, tusiitumikie dhambi tena."* (Waru. 6:3-6). Ubatizo ni ramani ya Mungu inayotumiwa na damu ya Kristo katika maisha yetu kwa ubatizo. Tunakuwa huru na dhambi zetu za zamani kama tu tukibatizwa.

Hii haimanishi "kunyunyiza. Andiko hilo hapo juu linasema ubatizo ni maziko. Hatuwezi kupeleka maiti makaburini, na kumwekea udongo kidogo juu yake; tunazika mwili.

Kama haujachuka maelezo haya, kwa nini usianze sasa?